

## **Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDFF)**

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana tangu 2015 hadi 2020 ni kuboreshwa kwa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, maji, ajira na miundo ambao imechochea maendeleo kwa wananchi.

Hatua hiyo imetokana na uongozi makini wa Serikali wa viongozi wa Serikali mbili zinazounda Muungano ambao ni Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Dkt. Ali Mohamed Shein ambao wamesimamia kikamilifu miradi inayotekelezwa kupitia Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo (CDFF).

Mfuko huo ulianzishwa kwa lengo la kuchochea maendeleo ya majimbo ya uchaguzi ya Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Sheria Na. 16 ya Mwaka 2009 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Katika kutekeleza miradi hiyo kiasi cha sh. 6,843,925,860 zilizopelekwa Zanzibar zimenufaisha wananchi katika sekta za Afya, Maji, Ajira, Elimu na Miundombinu.